


## MADINI YA RISASI “YA KUPELEKWA NYUMBANI”

Madini ya Risasi hupelekwa nyumbani kutoka kazini katika Nguo, Viatu, na Magari



### Familia Yako na Risasi “Ya Kupelekwa Nyumbani”

Madini ya risasi iyaaweza kusababisha matatizo ya afya kwa watoto na watu wazima. Wanawake wajawazito na ambao wananyonyesha, na watoto wadogo wanaweza kuathirika kwa urahisi na wanafaa kupimwa.

#### Watu wote Wazima

- Kuchoka na Kuumwa na kichwa
- Maumivu ya misuli na fundo
- Kubadilika kwa hisia na hamu ya kula
- Ubongo, neva na figo kuharibika
- Matatizo ya uzazi kwa wanaume na wanawake
- Kupunguka kwa hamu ya kufanya ngono

#### Wanawake Wajawazito

- Kupoteza Mimba
- Kuzaa mtoto kabla ya wakati
- Watoto wenye uzito mdogo wanapozaliwa
- Kijusi kuharibika kabisa

#### Wanawake Ambao Wananyonyesha

- Huenda wakawa na maziwa yaliyoathirika yanayoweza kumwathiri mtoto na risasi

#### Watoto

- Kuharibika kabisa kwa afya ya ubongo, neva na figo
- Matatizo ya kudumu ya kujifunza
- Matatizo ya kukumbuka mambo

### MADINI YA RISASI “YA KUPELEKWA NYUMBANI” NI

**Vumbi ya madini ya risasi inaweza kuletwa nyumbani kutoka kazini**

Madini ya risasi ya kupelekwa nyumbani hutoka wakati vumbi ya madini ya risasi iliyozalishwa kazini imeletwa nyumbani katika nguo, viatu na vifaa. Inaweza kubebwa hadi kwenye gari, samani, sakafu, zulia na vifaa vingine vya mtu binafsi. Kutokana na haya, familia yako inaweza kuhatarishwa na risasi hata kama hakuna hatari za risasi nyumbani mwako.



### KUPUNGUZA MADINI YA RISASI “YA KUPELEKWA NYUMBANI”

**Ondoa vumbi ya madini ya risasi katika nguo, viatu na vifaa**

Ikiwa unafanya kazi ya kutumia madini ya risasi, chukua tahadhari hizi:

- Badilisha nguo na viatu vyako kabla ya kuingia kwenye gari lako
- Weka nguo chafu na viatu vya kazini kwenye mfuko wa plastiki
- Nawa mikono na uso kabla ya kuondoka kazini
- Osha nguo za kazi kando na ububujishe maji tu kwenye mashine ya kufulia bila nguo, kabla ya kuosha nguo zingine

### ILI KUJIKINGA NA MADINI YA RISASI KAZINI

**Jikinge kutokana na madini ya risasi kazini**

- Usile, kunywa, kuvuta sigara au kubadilisha nguo kazini
- Hakikisha kucha na nywele za uso ni safi na hazina vumbi



# MADINI YA RISASI “YA KUPELEKWA NYUMBANI”

Kazi na Burudani Huenda Zikafanya Watu Wazima Wakahatarishwa na Madini ya

Ijapokuwa hatari za madini ya risasi zimejulikana kwa miaka mingi, vifaa vingi vya kawaida bado vina risasi. Kazi na burudani zingine huwaweka watu kwenye hatari kubwa ya kuathiriwa na risasi. Jua ikiwa kazi au burudani yako hukufanya uhatarishwe na risasi na uhakikishe umechukua tahadhari.



## Ujenzi

- Kupaka rangi au kuondoa rangi
- Kuunda upya na kukarabati
- Ufundi wa mabomba, kung'arisha, na kupanga matofali
- Kuchoma madini ya risasi
- Kujenga na kukarabati daraja, mnara wa tangi la maji, matangi
- Kuunganisha chuma au kukata vifaa kwa kutumia mseto wa madini ya risasi

## Burudani (upendayo kufanya)

- Kukarabati/kupanga nyumba tena
- Kuyeyusha madini ya risasi kwa ajili ya kifaa cha kuvulia, risasi, au vidude vya kuchezea
- Kulenga shabaha
- Kutumia ving'arishaji vya risasi kwenye vyungu
- Kuchakata upya vyuma vilivyotupwa, na kukarabati rejeta
- Kuunda glasi zenye mapambo
- Kuchoma mbao zilizopakwa rangi

## Utengenezaji

- Betri zenye asidi ya madini ya risasi
- Kebo, bidhaa za waya, solda ya risasi
- Bunduki, risasi, vilipuzi
- Mpira au plastiki

## Ukarabati

- Kazi za magari au motokaa
- Kukarabati meli
- Kuunganisha vyuma, kukata, na kulainisha
- Kusaga mseto wa risasi au maeneo yaliyofunikwa na risasi
- Kuunganisha na kukarabati vifaa vya elektroni
- Ukarabati unaoathiri/kutawanya rangi yenye madini ya risasi

## Shughuli Zinazohusisha Metali

- Kukalibu madini, kalibu, kuponda vyuma
- Kusaga
- Kutengeneza na kuunda ili kutumia tena ubao wa umeme

## Vyanzo vingine

- Kuondoa vitu kwenye maeneo ya ufyatuzi
- Kutumia rangi, wino, pigmenti na ving'arisho vyenye risasi
- Kufanya kazi katika tanuri la kuchomea taka

